



TRC imeongeza Huduma ya Usafiri wa Abiria kwa treni ya Deluxe mara mbili kwa wiki kutoka Dar es Salaam (Alhamis Saa 2 Asubuhi na Jumapili Saa 4 Asubuhi) na kutoka Kigoma (Ijumaa saa 2 Usiku na Jumatatu Saa 2 Usiku)

TRC YAPOKEA VIPIMA ULEVI 11 ILI KUPUNGUZA AJALI ZA TRENI ZA MIZIGO NA ABIRIA



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe akabidhi vipima ulevi 11 kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa katika ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka ya Usafiri wa Nchi kavu na Majini - SUMATRA jijini Dar es Salam kwa lengo la kupunguza na kudhibiti ajali za treni zitokanazo na ulevi wa wafanyakazi wa treni za abiria na mizigo Oktoba 2018.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu. Masanja Kadogosa akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi vipima ulevi 11 kwa TRC katika ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini kwa lengo la kupunguza na kudhibiti ajali za treni zitokanazo na ulevi wa wafanyakazi wa treni za abiria na mizigo Oktoba 2018.



Baadhi ya Viongozi wa Shirika la Reli Tanzania - TRC, SUMATRA na TAZARA waliohudhuria hafla ya kukabidhi vipima ulevi 11 TRC na kwa lengo la kupunguza na kudhibiti ajali za treni zitokanazo na ulevi wa wafanyakazi wa treni za abiria na mizigo katika Makao Makuu ya Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini Oktoba 2018.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja adogosa akimuonesha Mkuu wa Majeshi Jenerali Venance Mabeyo Cheti cha Shahada kilichotunukiwa TRC na Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere kwa kutoa Huduma bora ya Usafiri wakati wa vita ya Kagera alipotembelea Ofisi ya Makao makuu ya TRC jijini Dar es Salaam Oktoba 2018.



Mhandisi kutoka Kampuni ya Yapi Merkezi (Kulia) akimuonesha Mkuu wa Majeshi nchini Jenerali Venance Mabeyo (Kushoto) mchoro wa ramani ya Stesheni ya reli ya kisasa - SGR inayojengwa eneo la Stesheni jijini Dar es Salaam Oktoba 2018.

Meneja Mradi wa SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Maizo Mgedzi (kushoto) akimuelezea Mkuu wa Majeshi nchini Jenerali Venance Mabeyo (wa tatu kushoto) ubora wa Reli ya Kisasa iliyotandikwa Soga Kibaha mkoani Pwani Oktoba 2018.



Wakazi wa kata ya Visegese wilayani Kisarawe mkoa wa Pwani wakiwa nje ya kituo cha malipo ya fidia ya ardhi na Nyumba ili kupisha Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR uliopita kwenye maeneo yao Oktoba 2018.



Maofisa wa Shirika la Reli Tanzania - TRC wakiendelea na zoezi la ulipaji fidia ya ardhi na nyumba ili kupisha Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR katika kata ya Visegese Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani Oktoba 2018.



Viongozi wa Shirika la Reli Tanzania kutoka Idara tofauti wakiwa katika zoezi la kurejesha maeneo ya hifadhi ya reli yaliyovamiwa na wananchi kwa shughuli za kibinadamu eneo la Kurasini Mivinjeni katika Wilaya ya Temeka jijini Dar es Salaam mapema mwezi Oktoba 2018.



Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania wakiendelea na kazi ya kuzungushia uzio eneo la Hifadhi ya reli iliyovamiwa na wananchi kwa shughuli za kibinadamu Mivinjeni Kurasini katika wilaya ya Temeka jijini Dar es Salaam ili kuhakikisha eneo hilo halivamiwi tena na wananchi Oktoba 2018.



Sehemu ya eneo la Hifadhi ya reli iliyovamiwa na wananchi kwa shughuli za kibinadamu ikiwa imezungushiwa uzio wa Mataruma Mivinjeni Kurasini katika wilaya ya Temeka ili kuhakikisha eneo hilo halivamiwi tena na wananchi Oktoba 2018.



Mhandisi kutoka Kampuni ya Yapi merkezi (wa pili kulia) akiwaelezea Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Uganda Bwana Charles Kateeba (wa kwanza kulia) na Ujumbe wake ujenzi wa Reli ya Kisasa walipotembelea kambi ya SGR Soga Kibaha kwa lengo la kuona maendeleo ya Ujenzi pamoja na kujifunza Oktoba 2018



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli nchini Uganda Bwana Charles Kateeba pamoja na ujumbe wake wakitazama kazi ya utengenezaji Mataruma ikiendelea katika kiwanda cha kuzalisha Mataruma kilichopo kambi ya Soga Kibaha mkoani Pwani lengo la kujifunza namna ambavyo serikali ya Tanzania imeweza kutekeleza mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa Oktoba 2018.